**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO**


Mawasiliano:
Anuani ya simu.
Simu: **0755 773876/0714 637073**
**Barua pepe: kibedyasec@gdc.go.tz**

Ofisi ya Mkuu wa Shule
Shule ya Sekondari Kibedya
S.L.P. 81,
**Gairo-Morogoro.**


---

Tarehe …………………

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………..**
**……………………………………………**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIBEDYA, HALMASHAURI YA WILAYA YA GAIRO -MKOA MOROGORO KWA MWAKA ………….**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………. na atasoma tahasusi ya …………

Shule ya Sekondari KIBEDYA ipo umbali wa Kilometa 10 kutoka Stendi ya Mabasi Gairo, Usafiri kutoka stendi unapatikana ,Nauli ni Shilingi 5000/- kwa pikipiki na Shilingi 4000/- kwa usafiri wa umma.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe …………….. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………………… Mwisho wa kuripoti ni tarehe ...........

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni shati nyeupe 2 za mikono mirefu aina ya tomato, suruali nyeusi 2 za kitambaa zisizo na marinda, urefu wake ziguse kiatu, zipindwe chini na upana wa chini uwe (size 14)
ii. Tai ndefu ya rangi nyeusi
iii. Sare ya Michezo ni Raba nyeupe,track suit moja(1) ndefu ya bluu (dark blue).
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule;
vi. Masweta mazito mawili(2) rangi ya kijivu .
vii. Tisheti (T-shirt) rangi ya bluu (Dark blue) inapatikana shuleni.

**Nguo za kushindia.**

1. Suruali ndefu mpaka chini kwenye kifundo cha mguu rangi ya ugoro (brown) mbili pamoja na tshirt ya kijivu isiyo na maandishi yoyote (aina ya manga).
2. Viatu vyeusi vya kufunga (raba) jozi moja(1) na slipers nyeusi.
3. Nguo za ndani za kiume (boxer) zisizopungua tano (5).
4. Singland Zaidi ya mbili (2) nyeupe za kuvaa ndani ya shati.
5. Masweta meusi mazito mawili (02)
6. Pulneck nyeupe mbili (02)

**Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 12,counter book 4qr .
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha Imeabatishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator (function 991)
vi. Godoro la futi $\mathbf{2\frac{1}{2} \times 6}$
vii. Mashuka Jozi 2,(rangi ya light blue) blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 ya duara rangi nyeupe.
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko na ndoo kubwa 1 (lita 20 yenye mfuniko)
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 (soft broom 1 &hard broom 1)
xi. Ruber squizer 1(mopper)
xii. Graph pad 02 Kwa kila mwanafunzi
xiii. Taa ya sola- Kwa ajili ya matumizi ya kujisomea umeme unapokatika
xiv. Disposable gloves 1 box Kwa wanaosoma PCB
xv. Laboratory coat Kwa wanaosoma PCB

## 2.1 Michango mbalimbali

**a) Michango ifuatayo ilipwe kwenye akaunti ya shule,NMB A/C NA.24010000614 (KIBEDYA SECONDARY SCHOOL).Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in slip ya bank.**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari. na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa;
x. Kusababisha mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha mbili (2) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**.........................**
**MOHAMEDI NEHEMIAH ABELI**
**MKUU WA SHULE**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO**: -

**Mkuu wa Shule: 0714637073/0755773876**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0714146416/0697963433**

**Patron: 0767245499**

**Mhasibu- 0755622313**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI YA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**

**A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI:**

- JINA LA MWANAFUNZI ________________________________________
- TAREHE YA KUZALIWA________________
- MAHALI ULIPOZALIWA (MKOA NA WILAYA) _____________
- MAHALI UNAPOISHI _____________________________________________
- URAIA ________________
- SHULE ULIYOTOKA _________________________________________
- NAMBA YA MTIHANI (CSEE) _________________

**B. TAARIFA YA MZAZI AU MLEZI:**

- JINA LA MZAZI/ MLEZI_____________________________________________
- KAZI YA MZAZI/ MLEZI __________________________________________________
- ANUANI YA MZAZI/ MLEZI __________________________________________________
- NAMBA YA SIMU YA MZAZI/ MLEZI _________________________________________

  JINA NA NAMBA YA SIMU YA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI

  (i) JINA__________________________

  NAMBA YA SIMU________________

  (ii) JINA_________________________

  NAMBA YA SIMU________________

- BARUA PEPE (EMAIL ADRESS) YA MZAZI/ MLEZI KAMA IPO_______________________________

C. KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA:

Mimi______________________________.Kidato cha_________Mwaka_______Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote, nakubali kuipokea / sikubali kuipokea nafasi niliyopewa,nathibitisha kwamba nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa. Naahidi kuyazingatia.

Tarehe______________________________Saini___________________

**D.KUKUBALI SHERIA ZA SHULE**

MWANAFUNZI

Mimi_______________________________nimezisoma nakuzielewa sheria na ninaahidi kwamba nitazingatia sheria za shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule,nikikiuka sheria hizo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa kanuni,taratibu na sheria zilizopo.

Tarehe _______________Saini _______________

**E. MZAZI (AJAZE SEHEMU HII)**

**MZAZI**

i. Mimi mzazi/mlezi wa ___________________________ nimeleewa maagizo na ninapenda ifahamike kuwa dini ya mwanangu ni _________________________ na dhehebu lake ni _______________________.

ii. Ninaruhusu mwanangu kushiriki katika makongamano au warsha za kidini nje ya shule hususani zile zinazofanyika nje ya mkoa wa Morogoro anapokuwepo na mwalimu mlezi wa shule hii.

iii. Ninaruhusu likizo fupi atoke shuleni na kwenda kwa _________________________________ Uhusiano wake na mwanangu ni _____________________ namba yake ya simu ___________

iv. Aidha,mimi _____________________________________ ambaye ni mzazi nimesoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi _____________________________ na ninaahidi kutimiza wajibu wangu nikiwa mzazi /mlezi wa mtoto huyu kwa kumshauri ipasavyo pamoja na kutimiza mahitaji yake ya shule.

JINA LA MZAZI/MLEZI ………………………………………

SAINI YA MZAZI/MLEZI……………………………………….

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**Student name ___________________________Date ___________Signature _____________**

**PART A:**

**From The Headmaster,**
**Kibedya Secondary School,**
**P.O.Box 81,**
**Gairo-Morogoro**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

**Please examine the above-named student as to her physical and mental fitness for a full-time student. The examination should include the following category (a-d)**

a) **(i) Eyesight (ii) Hearing (iii) Speech (iv) Limbs (v) Venereal diseases (vi) Leprosy (vii) Epilepsy**
b) **Neurosis**
c) **Other serious diseases e.g. Asthma, T.B etc.**

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE**

**(To be completed by Government Medical Officers) I have examined the above named student and consider that he is fit/unfit for full time studies.**

i. **Eyesight__________________________________________________________**
ii. **Hearing____________________________________________________________**
iii. **Speech ____________________________________________________________**
iv. **Limbs _____________________________________________________________**
v. **Venereal diseases__________________________________________________**
vi. **Leprosy____________________________________________________________**
vii. **Epilepsy__________________________________________________________**
viii. **Neurosis _________________________________________________________**
ix. **Other serious diseases**
   a) **Asthma_______________________________________________________**
   b) **T.B _________________________________________________________**

**Other comments:**

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

_________________________________________________________________

**Name ____________________________ Date ______________ Signature ________________**

**STATION ___________________________DESIGNATION _______________________**

**N.B.I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.**

## KIBEDYA SECONDARY SCHOOL

## A- LEVEL SUGGESTED BOOK REQUIREMENTS

**GEOGRAPHY BOOKS**

1.Waugh D (2009) Geography an Intergraded Approach, Nelson Thomas Uk

2.Leongh C.G and Morgan C. Gillian (1972) Human and Economic Geography Second Edition Oxford

3.Bunnett R.B(1973) General Geography In Diagram Longman

4.Pritchard J.M And Munowenyu E (1988) A Certificate Geography Of Zimbabwe Longman Zimbabwe Ltd

5.Ahmed Rubwama (2013) Elementary Physical Geography

6.Daniel Sagatha (2014) Practical Geography for East Africa

**7.** Pritchard J.M Practical Geography

**VITABU VYA KISWAHILI**

1. Kiswahili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano na sita (lugha na sarufi) TET
2. Kiswahili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano na sita (fasihi) TET
3. Tahakiki ya Kiswahili II

**Vitabu vya fasihi**

**A: Tamthilia**

- Kivuli kinaishi (Said Mohamedi)
- Morani (Emmanuel Mbogo)
- Nguzo mama (Penina Mhando)

**B: Riwaya**

- Vuta n'kuvute (Shafi A. Shafi)
- Mfadhili (Hussein Tuwa)
- Kufikirika (Shaban Robert)
- Usiku utakapo kwisha (Mbunda Msokile)

**C: Ushairi**

- Chungu tamu (Theobard Mvungi)
- Fungate ya uhuru (Mohamedi Seif)
- Kimbunga (Haji Gora)

**HISTORY BOOKS**

1. Contemporary Historical Events (Paper 1 And Paper 2) By Mwalimu Shibitali Ck Tumaini
2. Essentials In Advance Level History (Paper 1 And Paper 2) By Saleh Yassin
3. Mastering Advanced Level History (Paper 1 And Paper 2) By Mwalimu Kato Abubaker Kassim

**CHEMISTRY BOOKS**

1.General Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
2.Physical Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
3.Organic Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
4.Inorganic Chemistry By Tanzania Institute Of Education(Tie)
5.Ngaiza,A Level Chemistry Series
6.Unga ,A Level Chemistry Series
7.A Level Chemistry Practical By R.S. Mlungu

**BIOLOGY BOOKS**

- Biology Student Book Form Five by Tanzania Institute of Education (Tie)
- Biology Student Book Form Six by Tanzania Institute of Education (Tie)
- Complete Advanced Biology Form Five by Respicius Rwehumbiza
- Complete Advanced Biology Form Six by Respicius Rwehumbiza
- Understanding Biology
- Biological Science (Bs)

**PHYSICS BOOKS**

1. Physics for Advanced level secondary school, students book form five by TIE
2. Physics for Advanced level secondary school, students book form six by TIE
3. Principles of physics for class XI, V.K Mehta, S.Chand
4. Modern ABC of physics for class XI part I &II by Satish K. Gupta
5. Modern ABC of physics for class XII part I & II by Satish K. Gupta